

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 6 WA WANAHISA WA NATIONAL INVESTMENTS PLC (NICOL)

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 6 wa mwaka wa Wanahisa wa National Investments Plc (Nicol) utafanyika siku ya Jumamosi, tarehe 21 Novemba, 2020 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa (JNICC), uliopo mtaa wa Shaban Robert, Dar es Salaam, Tanzania kuanzia saa 4:00 asubuhi. Ajenda ya Mkutano ni kama ifuatavyo:

- 6.1. MATANGAZO NA AKIDI
- 6.2. KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO
- 6.3. KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 5 ULIOFANYIKA TAREHE 26 OCTOBA 2019.
- 6.4. YATOKANAYO NA MKUTANO WA 5 WA WANAHISA
- 6.5. KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2019.
- 6.6. TAMKO LA GAWIO LA NUSU MWAKA KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA 2020.
- 6.7. KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI.
- 6.8. KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2020
- 6.9. KUPOKEA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MABORESHO KATIKA DAFTARI LA ORODHA YA HISA.
- 6.10. MENGINEYO.


### MAELEZO MUHIMU:

Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria mkutano ni lazima wawasilishe nyaraka zifuatazo: nakala ya stakabadhi yake ya Hisa (Depository Receipt) pamoja na Kitambulisho cha Kitaifa au kitambulisho cha mpiga kura au pasipoti.

Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi za NICOL zilizopo Mikocheni B, 11 Serengeti Road (kwa njia ya mkono au barua pepe [invest@nicol.co.tz](mailto:invest@nicol.co.tz)) kabla ya saa 4 asubuhi Ijumaa ya tarehe 20 Novemba 2020.

Fomu ya uwakilishi (Proxy forms) itakua inapatikana katika ofisi za NICOL au unaweza kuzipakua katika tovuti ya NICOL's ([www.nicol.co.tz](http://www.nicol.co.tz)).

Kwa idhini ya Bodi



Arphaxad GA Masambu  
CEO/ Katibu wa Kampuni